

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**  
**Halmashauri ya Manispaa ya Lindi**

Telegraphic address: "Mkurugenzi  
wa Manispaa"  
**Tel: 023-220-2164**  
**Fax: 023-2202116**  
E-mail: info@lindimc.go.tz



Ukumbi wa Manispaa,  
S.L.P.1070  
**LINDI**

Kumb.Na.LMC/A.50/19VOL.III/18

21/01/2021

**TANGAZA LA UTOAJI WA MIKOPO YA ASILIMIA KUMI (10%) YA MAPATO YA  
NDANI YA HALMASHAURI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, anapenda kuvitangazia vikundi vyote vya Wajasiriamali vilivyopo ndani ya Manispaa ya Lindi, Ofisi yake imeanza kupokea maombi mapya ya mikopo inayotokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Mikopo hii itatolewa kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu vitakavyokidhi sifa zilizoainishwa hapa chini.

**SIFA ZA VIKUNDI VITAKAVYOOMBA MKOPO NI PAMOJA NA;**

- 1) Kikundi kiwe kimetambuliwa kama kikundi cha Wanawake, Vijana au Watu wenye Ulemavu na kupewa cheti cha Utambuzi na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi
- 2) Kikundi kiwe kinajishughulisha na Ujasiriamali au kinakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati.
- 3) Kwa vikundi vya Wanawake au Vijana idadi ya wanakikundi ianzie 10 na kuendelea na kwa vikundi vya Watu wenye ulemavu idadi iwe kuanzia watu 5 na isizidi 10.
- 4) Kikundi kiwe kina akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya kikundi
- 5) Wanakikundi wawe ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
- 6) Kikundi kisiwe na wajumbe wenye ajira rasmi.

- 7) Kwa vikundi vilivyowahi kukopa na havijamaliza kulipa madeni yao na vinahitaji mkopo, vihakikishe vinamaliza mikopo ya nyuma ili wawe na sifa ya kukopa tena
- 8) Kwa vikundi vyenye madeni ya mikopo ya nyuma, maombi mapya hayatapewa kipaumbele mpaka watakapomaliza kulipa madeni ya0.
- 9) Maombi yote yaambatanishwe na Katiba ya kikundi, cheti cha utambuzi wakikundi pamoja taarifa ya usuluhisho wa kibenki (Bank Statement).
- 10) Kwa vikundi vinavyojishughulisha na biashara, leseni ya biashara na nakala halisi ya taarifa ya akaunti kutoka katika benki ambayo kikundi kina akaunti, barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Mtaa na Kata pamoja na wazo la biashara.
- 11) Nakala halisi ya utambulisho wa kikundi kutoka kwa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji kwa kadri itakavyokuwa na Mtendaji wa Kata
- 12) Nakala halisi ya Wazo la Biashara.

Maombi yatakayofanyiwa kazi ni yale yatakayokuwa yamezingatia vigezo vilivyoainishwa hapo juu. Aidha, maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, yakiwa yameidhinishwa na Mwenyekiti wa Mtaa, Mtendaji wa Mtaa na Mtendaji wa Kata husika.


Vikundi vinavyohitaji mikopo na vyenye sifa zilizoainishwa hapo chini, vinatakiwa kuwasilisha maombi yao kuanzia tarehe ya tangazo hili na mwisho ni tarehe 15/02/2021 saa 9:30 alasiri.

**Vikundi ambavyo viliwahi kutuma maombi ya mikopo bila kuzingatia maelekezo tajwa hapo juu, vitalazimika kurejea mchakato wa maombi upya sawa na tangazo hili.**

Kwa maelezo zaidi, fika Ofisi za Idara ya Maendeleo ya Jamii zilizopo nyuma ya uwanja wa Ilulu au piga simu Na. 0787962310 au 0658 962310 au 0787 313 923.

**Ninawatakia ushiriki mwema**

  
Satura J.M,  
Mkurugenzi wa Manispaa,  
LINDI

  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
LINDI